# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

“MET Opp. Maweni Hospital,
S.L.P. 880,
47115 KIGOMA,
Barua Pepe: rbckigoma@pccb.go.tz.
**TANZANIA.**
www.pccb.go.tz

**KIGOMA - APRILI 14, 2020**

## TAARIFA KWA UMMA

## KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

## TAKUKURU (M) KIGOMA YAOKOA ZAIDI YA SHILINGI MILLIONI SITINI NA SABA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI HADI MACHI 2020

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Kigoma imefanikiwa kuokoa fedha kiasi cha **shilingi 67,468,800/=** katika kipindi cha Januari hadi Machi 2020. Fedha hizo zimeokolewa kutokana na Operesheni mbalimbali za uchunguzi zilizohusisha chama cha Ushirika cha RUMAKO kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, Chuo cha Uganga Maweni pamoja na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo.

Kati ya fedha hizo, fedha kiasi cha **shilingi 48,578,400/=** ziliokolewa katika Chama cha Msingi cha RUMAKO baada ya kufanyiwa ubadhilifu na viongozi wa chama hicho kwa kujikopesha bila kuzirejesha pamoja na manunuzi ya pembejeo hewa.

Fedha kiasi cha **shilingi 3,140,000/=** ni fedha za ada zilizolipwa na wananchi katika chuo cha Uganga Maweni kwa ajili ya kupata mafunzo ya usimamizi wa maduka ya madawa tangu mwaka 2015 bila kupata mafunzo hayo. Fedha hizo zimeokolewa na kukabidhiwa kwa wananchi waliokuwa wanadai fedha zao.

Aidha TAKUKURU imeweza kuokoa fedha kiasi cha **shilingi 14,225,400**/= katika ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo ambapo iliweza kusitisha malipo yaliyokuwa yameandaliwa kulipa kazi ambazo hazikufanyika.

Kiasi kingine cha fedha kiasi cha **shilingi 1,525,000/=**ziliokolewa kutoka katika kazi za uchunguzi zilizohusisha Idara ya Uhamiaji na Mali asili.

**UCHUNGUZI:**

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Katika kipindi cha Januari hadi Machi 2020, TAKUKURU (M) Kigoma imepokea jumla ya malalamiko115 ya vitendo vya rushwa ambayo yanaendelea kufanyiwa kazi katika hatua mbalimbali. Idara zinazolalamikiwa zaidi ni pamoja na Mamlaka za serikali za mitaa (Watendaji wa kata vijiji na mitaa), Vyama vya kuweka na kukopa (SACCOS), Baraza la nyumba na Ardhi pamoja na vyama vya ushirika (AMCOS).

Jumla ya kesi 3 zimefunguliwa katika kipindi cha Januari hadi machi 2020 na zinaendelea kusikilizwa katika hatua mbalimbali.

TAKUKURU Mkoa wa Kigoma katika kipindi cha Aprili -Juni 2020 itaendelea kufanya uchunguzi wa  ubadilifu wa fedha kiasi **shilingi 19,522,494.60** za Mauzo ya kahawa za wakulima kwa mwaka 2015/2016 katika Chama cha Msingi MANYOVU AMCOS Wilaya ya Buhigwe na kuchukua hatua za kisheria,

**UZUIAJI RUSHWA:**

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

TAKUKURU (M) Kigoma imeendelea kufanya uchambuzi wa mifumo ambapo katika kipindi cha Januari – Machi 2020 uchambuzi uliofanywa ulijikita katika utendaji wa vyama vya ushirika AMCOS lengo likiwa ni kubaini mianya ya rushwa na kushauri mamlaka husika jinsi ya kuziba mianya hiyo.

Kupitia uchambuzi huo TAKUKURU iliweza kubaini yafuatayo:-

- Ucheleweshaji wa malipo ya wakulima,
- Makato makubwa ya marejesho ya mikopo ya pembejeo isiyoendana na mikopo halisi waliyopewa wakulima,

- Ubadhirifu wa mali za vyama vya ushirika pamoja na
- Ukosefu wa uwazi katika uendeshaji wa vyama vya ushirika.

(a) **UFUATILIAJI WA MIRADI YA MAENDELEO**:

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Katika kipindi cha Aprili – Juni 2020 TAKUKURU itaendelea kufanya vikao vya kiutendaji vyenye lengo la kuwekeana maazimio na mikakati ya kuondokana na mianya ya rushwa iliyobainika.

Aidha ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri za Mkoa wa Kigoma, umefanyika ili kuhakikisha kuwa inatekelezwa kwa viwango na kwa wakati.

Katika kipindi cha Januari hadi Machi 2020 miradi ya Elimu na Afya, yenye thamani ya **shilingi 479,219,105**/= imefanyiwa ufuatiliaji.

Kupitia ufuatiliaji wa miradi hiyo TAKUKURU iliweza kusitisha malipo yenye thamani ya **shilingi 14,000,000/=** ya mradi wa ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule ya Msingi Nyansimbi pamoja na **shilingi 225,400/**= za ujenzi matundu 6 ya vyoo katika shule ya Msingi Mwamila zilizopo katika wilaya ya Uvinza baada ya kubaini kuwa kazi hizo hazikufanyika licha ya malipo hayo kuandaliwa.

Katika kipindi cha Aprili - Juni 2020 ufuatiliaji wa miradi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa utaendelea ili kuhakikisha inatekelezwa kwa viwango vinavyotakiwa

**UELIMISHAJI UMMA:**

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Katika kipindi cha Januari – Machi 2020 jumla ya wananchi 19,301 kutoka makundi mbalimbali walipatiwa elimu kuhusu madhara ya rushwa na kuwahamasisha kushiriki kikamilifu katika kukemea, kufichua na kujitokeza kutoa ushahidi wa vitendo au viashiria vya rushwa.

Katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2020 TAKUKURU Mkoa wa Kigoma itaendelea kuwahamasisha wananchi kushiriki katika kuzuia vitendo vya rushwa katika maeneo wanayoishi ambapo mkazo wa uelimishaji utajikita katika kuelimisha jamii kuhusu madhara ya rushwa katika uchaguzi.

Uelimishaji huo utaenda sambamba na ufuatiliaji wa viashiria vya rushwa katika mchakato wa uchaguzi mkuu, kuchunguza na kuchukua hatua dhidi ya watu watakao jihusisha na vitendo vya rushwa

**WITO:**

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

TAKUKURU inatoa wito kwa, wananchi wote kushiriki katika mapambano dhidi ya Rushwa wakati wote hususani katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu, kwa kuwaibua wala rushwa, Kukataa kujihusisha na vitendo vya rushwa na kushiriki katika kutoa elimu kwa wengine juu ya madhara ya rushwa katika jamii na kukemea vitendo vya rushwa vinavyofanyika katika maeneo yao.

Vilevile TAKUKURU inawafahamisha wananchi wa Mkoa wa Kigoma kuwa kumezuka wimbi la Matapeli wanaopiga simu na kujifanya Maafisa wa TAKUKURU au Idara nyingine za serikali kwa lengo la kuwarubuni. Hivyo wananchi kamwe wasikubali kutuma fedha kwa matapeli hao au kukutana nao nje ya ofisi bali watoe taarifa mapema katika ofisi zetu ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

Wananchi wanahimizwa kuwasiliana na ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Kigoma, ofisi za Wilaya Kasulu, Buhigwe, Uvinza,Kakonko na Kibondo kwa kufika ofisini au kupiga Simu ya Bure 113 inayopatikana kupitia mitandao ya TTCL, AIRTEL, VODACOM, TIGO, HALOTEL.

**Imetolewa na:**

Nestory Gatahwa
KAIMU MKUU WA TAKUKURU (M)
KIGOMA